Madondoo toka kitabu:

Hili ni Neno Langu

A na Ω

Injili ya Yesu

Ufunuo wa Kristo unaojulikana na wakristo halisi wa dunia nzima

Madondoo toka kitabu cha Gabriele,
nabii na mjumbe wa Mungu:

Hili ni Neno Langu
A na Ω

Injili ya Yesu

Ufunuo wa Kristo
unaojulikana na wakristo
halisi wa dunia nzima

(Kitabu hiki kinapatikana katika lugha ya kifaransa na ya kiingereza)

First Edition in Swahili: September 2022
1ère édition en Swahili: Septembre 2022

Translated from the original German title:
Traduit de l'allemand, titre original:

Das ist Mein Wort A et Ω

The German edition is the work of reference
for all questions regarding the meaning of the contents
Pour toute question se rapportant au sens,
l'édition allemande fait référence

© All Rights Reserved / Tous droits réservés
Gabriele-Verlag Das Wort GmbH

UTANGULIZI

Imepita sasa miaka elfu mbili, tangu Yesu wa Nazareti alipotabiri: «Wakati Roho wa ukweli atakapokuja, atawaongoza katika ukweli wote.» Hayo ndiyo yaliyofanyika na inayoendelea kutendeka kupitia Gabriele, nabii na mjumbe wa Mungu wakati wetu huu.

Katika kitabu chake kikubwa cha ufunuo, «*Hili ni Neno Langu. Alpha na Omega. Injili ya Yesu. Ufunuo wa Kristo unaojulikana na wakristo halisi wa dunia nzima*», Kristo Mwenyewe anaeleza kwa namna pana ukweli kuhusu maisha na mafundisho ya Mnazareti. Kristo anakosoa mafundisho potovu, anatueleza mambo yaliyokuwa yamefichwa hadi sasa, na ya ziada tena, «Ukweli wote», kama Alivyoahidi wakati alipokuwa kimwili katika Yesu.

Brosha hii inakusanya
madondoo kadhaa kutoka kitabu hicho
chenye kurasa zaidi ya 1000,
«Hili ni Neno Langu»

Yesu wa Nazareti alifundisha na kuishi Amri za Mungu

Mimi, Kristo, nilizaliwa katika mwili wa Yesu na nikawa Mwana wa mtu. Nilikuja kuonyesha wanadamu njia inayoongoza nje ya dhambi na utumwa. Katika Yesu wa Nazareti, nilifundisha Sheria ya Mungu na nikatoa mfano wa utekelezaji wa Sheria maishani mwangu. (...)

Nilifundisha upendo kati ya watu, upendo kwa wanyama, heshima ya mazingira na kutambua dunia kama mama ambaye wanae binadamu wanaishi na kutenda kazi humo. Nilifundisha usawa, uhuru, umoja, undugu na haki.



Yule anayemfuata Yesu Kristo, ni mfano kwa watu wengi

...Na wakachagua wawili wao Barsabe na Matiasi na wakaomba: «Oh! Mungu, wewe unayefahamu mioyo ya watu wote, tuonyeshe ni yupi kati ya hao wawili uliyemchagua kushiriki kwenye meza duara ya mitume ambapo ulimuinua mtume wako Petro ili awe kiongozi chetu.» (Sura. 96, 1-3)

Mimi, Kristo, ninaeleza, ninarekebisha na ninatafsiri maneno kwa kina:

Sijawahi kamwe kuinua mtu yeyote ili awe mchungaji wa walio wangu.

Kwa wale wote walionifuata – pia kwa Petro ambaye aliniuliza ni nani aliyepashwa kuwaongoza wengine, ninawaamuru haya: Aliye mkuu zaidi kati yenu na awe mdogo na yule aliyeweza kupokea nuru na nguvu zaidi. – kwa sababu ya maisha yake katika upendo wa Mungu – awe kwa watu wengi kama bango linalowaelekeza kwenye njia ya upendo wa Mungu.

Nimewachagua ninyi nyote kuwa wabeba nuru (...).

Kwa maana anayeruhusu ainuliwe na kutukuzwa haishi katika Roho Wangu; atashushwa.

Mafarisayo walikufuru matendo mema ya Yesu wa Nazareti

Na tazama, akaletwa kwake mtu aliyekuwa bubu, mwenye pepo. Na baada ya yule pepo kutolewa, yule bubu akaweza tena kusema. Watu wakashangaa na kusema: «Hakuna mtu aliyewahi kuona muujiza kama huu katika Israeli.» Lakini mafarisayo wakasema: «Anawafukuza pepo kwa uwezo wa pepo wakuu mno.» (Sura ya 24, 8)

Mimi, Kristo, ninaeleza, ninarekebisha na ninatafsiri maneno kwa kina:

Nilipochukua mwili katika Yesu wa Nazareti, nilitenda kazi mahali ambapo Baba yangu aliniweka. Kupitia nguvu za Baba, niliweza kuwaletea nafuu na uponyaji watu wengi na, kwa

uwezo wa Neno Hai, niliweza pia kuwaongoza kwenye dhamiri.

Hata hivyo, sikuweza kuwasaidia na kuwahudumia wote waliokuja Kwangu. Niliwekea mikono watu wengi ambao hawakupona. Vivyo hivyo, nguvu za giza nilizokemea ndani mwao hazikuacha kuwaandama. Kwani Sheria ya Uzima inasema: Mtapewa kwa kadiri ya imani yenu! Na: Nenda zako, na tangu sasa usitende dhambi tena! (...)

Mafarisayo wa leo wanatumia makufuru yale yale niliyotendewa hapa duniani katika Yesu wa Nazareti. (...) Baadhi ya Mafarisayo, wakiwa wamevaa mavazi ya kikuhani, wanasadiki kwamba wanabobea katika masuala ya imani. Ikiwa wanawashutumu jirani zao kuwa «watumishi wa shetani» au «watumishi wa Ibilisi», ni kwa sababu wao wenyewe wanamtumikia zaidi au kidogo kwa maisha yao na njia yao ya kufikiri.



Mlo wa Mwisho

Na wote walipokwisha kushiriki, aliwaambia: «Kila mara mnapojumuika kwa jina langu, toeni sadaka hii kwa ukumbusho wangu, andaeni mkate wa uzima wa milele, na divai ya ukombozi wa milele; vileni na vinyweni, kwa moyo safi, na mtapokea maada na uzima wa Mungu vilivyo ndani Mwangu.» (Sura ya 76, 25)

Mimi, Kristo, ninaeleza, ninarekebisha na ninatafsiri maneno kwa kina:

Nilitumia mkate na divai tu kama ishara za dhabihu ya mwili wangu na damu yangu. Hii ndiyo sababu hamungepashwa kuifanya sherehe bali kunikumbuka Mimi kila wakati, kupitia hisia, mawazo, maneno na matendo yenu.

Vivyo hivyo, mnapotumia zawadi za Uzima mlizopewa na Mungu kupitia Ardhi-Mama, mshukuruni wa Milele na kumbukeni tendo langu la ukombozi. Mkifanya hivyo kwa moyo safi, sio tu miili yenu ya kidunia itakayopokea maada ya kiroho au uzima wa kiroho, ila pia nafsi zenu. (Sura ya 76, 25).

Nilipochukua mwili katika Yesu wa Nazareti, nilimuomba sana Mungu, Baba yangu, na kuzungumza naye. Nilimwomba, Bwana, abariki chakula cha Karamu ya Mwisho na mitume wangu. Niliwaagiza haya: Ninachokifanya sasa, endeleeni kukifanya kwa ukumbusho wangu. Chakula ni kwa ajili ya mwili. Ninawapa chakula kama alama ya uthabiti wa kiroho. (Sura ya 76, 9)



Mateso na kifo cha Yesu wa Nazareti

Kwa nini Yesu mara nyingi aliweza kuwatoroka watesi wake na kwa nini haikuwa hivyo usiku ule? (Sura ya 76, 29-30)

Hadi leo, giza haikuwa na nguvu juu yangu kwa sababu mwili wangu wa kiroho ulikuwa safi. Nguvu za giza zilipata uwezo wa kuniteka Mimi, kwa sababu tu nilikuwa nimejivika mwenyewe makosa na mizigo ya uzao wa Daudi na familia nyingine, na hivyo nilionekana na nguvu za giza. (Sura ya 78)

Nguvu za giza zilisingizia, zikadhihaki na kuua mwili wangu, lakini hazikufanikiwa kufikia lengo lao: Kunitenga na Mungu kwa kunifanya niwe na shaka naye. Nilibaki ndani ya Baba na Baba alibaki ndani mwangu.

Hivi ndivyo nilivyomtukuza Baba ndani mwangu. Na hivyo ndivyo utukufu wa Baba ulikuja ulimwenguni katika nuru ya ukombozi kupitia Mimi, Kristo. Na hakuna awezaye kuzima nuru hiyo ya ulimwengu. Nuru hiyo ilitia nanga ndani ya nafsi zote na wanadamu wote, hata ndani ya pepo wakali wa giza. Wakubali

au la, wao pia walipokea nuru ya ukombozi kutoka kwangu. (Sura ya 82, 17-19)

Hata kama yeye [Pontio Pilato] aliosha mikono yake ili kuashiria kutokuwa na hatia, kwa kweli alianguka katika dhambi. Hakika, ingawa alikuwa na uhakika wa kutokuwa na hatia kwangu, alinitoa nife, mimi ambaye sikuwa na hatia. Kwa hiyo Pontio Pilato hakufaulu dhidi ya jaribu alilokabiliana nalo, kwa sababu alitoa maagizo kinyume na imani yake. Imani ya ndani haifai ikiwa hatutendi kwa mjibu wa imani. (Sura ya 81, 10-32)

Hivyo Pilato alidhihirisha udhaifu wake. Aliwaogopa watu kwa sababu alitaka kuhifadhi cheo chake duniani. Tabia ya Pilato ilikuwa na inabaki kuwa ishara kwa baadhi ya watu. Mtu mwenye mwelekeo wa kidunia hutegemea watu ili kudumisha uwezo na wadhifa wake duniani. Anafikia hatua ya kumtoa kafara jirani yake ili kudumisha utukufu na mamlaka aliyo nayo. (Sura ya 82, 3-4)

Maelezo kuhusu mafundisho ya Yesu Kristo

Yesu alienda Yerusalemu na akakutana na ngamia mwenye mzigo mzito wa kuni. Ngamia hakuwa na uwezo wa kuupandisha mzigo kwenye kilele cha mlima, na mwenye ngamia alikuwa akimpiga na kumtusi kikatili, bila kumsukuma mbele.

Yesu alipoona hayo, akamwambia: «Mbona unampiga ndugu yako? Na yule mtu akamjibu: «Sikujua kuwa huyu ni ndugu yangu.» Je! Huyu si mnyama wa kubeba mizigo mwenye mafaa tu ya kunitumikia?»

Na Yesu akamjibu: «Je si Mungu huyo mmoja ndiye aliyeumba kwa maada moja mnyama huyu na wanao wanaokusaidia, na hamkupokea wote wawili pumzi ya uhai toka kwa Mungu?»

Mtu huyo alishangaa sana kusikia maneno haya. Akaacha kumpiga ngamia na akampunguzia mzigo wake. Kwa hiyo ngamia akapanda mlimani, na Yesu akatembea mbele yake, naye hakusimama siku nzima.

Ngamia alimtambua Yesu, kwa sababu alikuwa amehisi upendo wa Mungu ndani mwake. Na mtu huyo alitaka kujua zaidi kuhusu fundisho hilo, na Yesu alimfundisha kwa hiari, na akawa mmoja wa wanafunzi wake. (Sura ya 31, 10-16)

Mimi, Kristo, ninaeleza, ninarekebisha na ninatafsiri maneno kwa kina:

Nilipochukua mwili kama Yesu wa Nazareti, nilizungumza na watu wengi kuhusu Sheria ya Uzima, na hata pia kuhusu wanyama ambao, kama wanadamu, wanahisi maumivu, mateso na furaha. Kama vile mwanadamu ameamriwa kumpenda jirani yake bali siyo kumchukia, mwanadamu pia anapaswa kuwapenda wanyama na kuwajibika nao. (...)

Niliendelea kuwafundisha wanadamu kwamba wanyama pia ni viumbe vya Mungu ambavyo wanadamu hawapaswi kuvidharau bali kuvipenda. Anayewapiga na kuwatesa wanyama, siku moja atalazimika kupatwa na dhuluma hiyo hiyo au mambo yanayofanana na hayo, katika nafsi yake au katika mwili wake.

Na baadhi ya wazee na wataalamu wa sheria ya Hekalu walimwendea na wakamswali: «Kwa nini wanafunzi wako wanafundisha kwamba ni kinyume cha Sheria kula nyama ya wanyama, japo, kwa mjibu wa Amri za Musa, ni lazima wanyama watolewe kama dhabihu? (...)» (Sura ya 51, 12)

Mimi, Kristo, ninaeleza, ninarekebisha na ninatafsiri maneno kwa mina:

Musa hakuamuru wala kuidhinisha dhabihu ya wanyama. Lakini hakuingilia kati mapenzi ya kishetani ya wale waliotaka kula nyama. Aliwafundisha kwamba kula na kutoa dhabihu ya wanyama ni dhambi. (...)

Eleweni kwamba, wanyama huhisi kile ambacho mwanadamu anataka kuwafanyia.

Katika zama hii ya mabadiliko ambamo ninaeleza, kurekebisha na ninatoa tafsiri ya kina ya maneno, maudhui ya kitabu hiki, ukatili kwa wanyama na mimea umefikia kiwango cha kupindukia. Wanyama na mimea wanateseka kutokana na udhalimu wa wanadamu. Watu wengi hawaheshimu tena

maisha yao wenyewe au ya viumbe vyote. Mojawapo ya madhara ya tabia ya uharibifu ya wanadamu ni, kwa mfano, mvurugiko wa mikondo ya magnetisi. Kwa hiyo wanyama wengi hupoteza uwezo wao wa kujielekeza wenyewe, kama matokeo, hususan ndege wanaohama. Kutokana na athari ya uchafuzi wa mito, maziwa, bahari na hewa ya dunia, aina nyingi za wanyama na mimea zinatoweka. (...) (Sura ya 51, 11-13)

Kwa hivyo, mjihisi wenye kuunganishwa kiroho na viumbe vyote, na mawe na mimea yote, na ilindeni maisha mliyokabidhiwa! (...)

Msiharibu kamwe uhai wa mnyama. Elewa kwamba, mazingira – uzima wa viumbe – inakutunza. Matunda ya mashamba, ya bustani na ya misitu yangepaswa kukutosha. Msiharibu, kwa nia mbaya, maisha ya viumbe vilivyo chini ya miguu yenu, ya wanyama au ya mimea. (Sura ya 19, 9)



Epukeni utumiaji nguvu na jihadharini msimwage damu

Nyumba ya Mungu, hekalu la Roho Mtakatifu, ni mwili wa mwanadamu na nafsi inayotoka kwa Mungu na kukaa ndani mwake. Ndani ya nafsi mna upendo, hekima na haki ya Mungu. Hivyo Mungu anakaa ndani ya nafsi. Kwa hiyo, nafsi na mwili wa mwanadamu ni hekalu la Mungu. Mtu aingiaye kwa nguvu katika nyumba ya nyama na mifupa ya wenziwe kwa kuwafanyia jeuri, kwa kuwatisha, kwa kuwatendea kama watumwa, hata kwa kuwaua, anatenda dhambi dhidi ya Roho Mtakatifu. (...)

Ndiyo sababu, ni bora mikono na roho yako viwe safi, siyo kuviepusha wizi na uporaji. Hususan msitumie kamwe jeuri, iwe kwa wanadamu iwe kwa wanyama, na mjihadhari kumwaga damu yao. (Sura ya 38, 4)



Kanuni ya sababu na matokeo

Sheria ya milele na ya ulimwenguni pote inayotenda kazi ndani ya vyote, Sheria ya Mbinguni, haibadiliki kamwe. Ni Sheria ya aina zote za viumbe vyenye uwepo safi. Anguko ndilo lilitokeza sheria ya kupanda na kuvuna. Kanuni hiyo inaweza tu kurekebishwa na utekelezaji wa Sheria ya Milele kimatendo; bali haiwezi kuepukika. (...)

Kanuni ya kupanda na kuvuna itabaki kuwa halali hadi muda ambapo yote yaliyo kinyume na Amri za Mungu yatakaporekebishwa na kugeuzwa kuwa nguvu chanya, na tena wakati viumbe vyote vitakaporudilia tena uzima ndani ya Mungu ambamo vilitoka. (Sura ya 25, 8)

Mungu ametoa uamzi huru kwa viumbe vyote vya kiroho, kwa nafsi na watu wote. Kwa hiyo kila mtu yupo huru kukubali Amri za Uhuru na Uzima, yupo huru kuzitekeleza au kuzikataa na kutenda kinyume nazo. (...)

Mbegu nzuri hutoa mavuno mazuri, mbegu mbaya hutoa mavuno mabaya. Kila mtu anaweza kuchagua kwa hiari yake mbegu

anazopanda, mbegu nzuri, mbegu nzuri kidogo au mbaya. Kila mtu huvuna matunda aliyoyapanda mwenyewe, wala si jirani yake; mtu huvuna tu matunda ya kile alichopanda mwenyewe. Wanapokabiliwa na madhara ya sababu zao, watu wengi hawajui kwamba wanavuna tu walichokipanda wenyewe; wanaamini wao ni wahasiriwa wa ghadhabu ya Mungu.

Mungu ni upendo na hajui hasira. Anamwondolea mwanadamu dhambi zake, iwapo tu anazitubia, anazimkabidhi Mungu, kuzirekebisha na kutozirudilia tena. (Sura ya 31, 1-3)



Kufundisha hukumu wa milele ni kumdharau Mungu

Na baadhi ya mafarisayo (…) walimwuliza Yesu wakisema: «Ulisema nini? Kwamba Mungu atauhukumu ulimwengu? Na Yesu akajibu: «Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa na kumtuma Mwanawe duniani ili wote wanaomwamini wasipotee bali wawe na uzima wa milele. (…)» (Sura ya 12, 10-11)

Mimi, Kristo, ninaeleza, ninarekebisha na ninatafsiri maneno kwa kina:

Mungu hahukumu milele kamwe! Lakini, kwa kufikiri, kusema na kutenda kinyume na Amri za kimungu, mtu hujijengea mahakama yake mwenyewe ambayo inamukatia hukumu; hiyo ndiyo anaiita «hukumu wa milele». (…)

Lakini hampaswi kumwogopa Baba yenu wa Mbinguni, kwa sababu anawapenda! Badala yake, ogopa mawazo yako ya kiutu, maneno na matendo mabaya, kwa maana yanaweza kukuongoza kwenye «laana» ndefu!

Mungu ni upendo! Kwa hiyo usimwogope. (Sura ya 12, 10-11)

Na elewa kwamba Jehanamu si mahali bali ni hali ya maisha ya nafsi ambayo imejitoa kwa mambo iliyo kinyume na sheria ya Mungu, iliyojitoa kwa «mfalme wa giza». (Sura ya 17, 9-10)

Msiomboleze wafu wenu

Anayeomboleza wafu bado yupo mbali na uzima wa milele, kwa sababu anaona kifo kuwa mwisho wa maisha. (...)

Tambua kuwa uzima wa muda katika mwili wa mwanadamu sio Uzima wa nafsi. Nafsi ilijivika mwili kwa kuishi muda mfupi tu duniani ili irekebishe na kulipa katika maisha ya muda dhambi iliyotenda katika marudio tofauti ya umwilisho duniani. Dunia ni mahali pa mapito tu. (Sura ya 26, 10-11)



Upendo kwa Mungu na kwa jirani

Tambua kwamba anayemchukia jirani yake, kwa sababu yoyote ile, anamkataa Mungu. Na anayepingana na Mungu hayumo katika ukweli, katika utimilifu wa Sheria ya Mungu ambayo ni Sheria ya upendo. (Sura ya 90, 12)

Mtu asiyemkubali na kumkaribisha jirani moyoni mwake kwa sababu ana chuki dhidi yake, bali anayemkataa, anayemdharau au hata kumchukia, hamzingatii Baba wa Milele na hanijui Mimi, Mimi Kristo, Mungu. Mwana wa Baba. Wala mtu huyo hamjui jirani yake au kujitambua yeye mwenyewe pia, kwani ndani mwake pia anakaa Roho wa Baba wa Milele ambaye hamkubali kwa jirani yake wala kumkaribisha moyoni mwake. (Sura ya 50, 5-8)

«Usiwafanyie wengine yale usiyotaka wakutendee» maana yake ni: Kuwa macho katika kila wakati wa maisha yako ya hapa duniani ili kuwa na dhamiri timamu kuhusu hisia na mawazo yako. Hivyo utakuwa na uwezo wa kunikabidhi Mimi, Kristo, uovu wa kibinadamu ulio ndani mwako kwa wakati,

kusudi usije ukamtendee jirani yako kile ambacho kingekurudilia tena wewe. Unachomfanyia jirani yako, unanitendea Mimi, Kristo, na pia wewe mwenyewe (...).

Ingelikuwa heri kumheshimu jirani yako na kumtendea kulingana na Sheria ya Milele. Lakini, usimfanyie kile anachokuomba ikiwa kipo kinyume na Amri za Mungu. (Sura ya 35, 1-8)

Tambua kwamba si vema kudai wenzio kile usichokuwa tayari kukitoa wewe mwenyewe. Ikiwa unatarajia jirani yako akufanyie kitu, jiulize kwa nini usikifanye wewe mwenyewe? (...) Huna moyoni mwako yote unayodai kutoka kwa wengine. (Sura ya 27, 5-6)

Kuua jirani yako ni kuharibu hekalu la Mungu. Nafsi ya aliyeuawa haina tena uwezekano wa kulipa uovu wake au kukamilisha majukumu ya umwilisho wake hapa duniani.

Yeyote atakayemwua jirani yake, aliye hekalu la Mungu, au kumfanya auawe, atapatwa na mkasa huo huo au msiba kama huo. Hofu, maumivu, hofu na kifo pia vitampata. Saa ya

kufa kwake hatapata raha, kwa sababu nafsi ya mtu yule aliyemwua akiwa bado na mwili wa kidunia na ambaye bado hajamsamehe itasimama mbele yake. (Sura ya 49, 4)

Mtu anayejiacha atawaliwe na wengine, na kwa sababu hiyo anatenda tu kile wanachomuambia, hata kama anagundua kuwa hayo hayalingani na mpangilio wake wa maisha, «huishi» kwa niaba ya wengine na hukosa maisha yake mwenyewe hapa duniani. Hanufaiki na siku zake; anatumiwa na watu hao anaotawaliwa nao. Ndio maana hajui njia anayopaswa kufuata hapa duniani. Mtu anayewafunga wanadamu wenzake kwake kwa kuwalazimisha mapenzi yake analinganishwa na kizuu anayehuchukua nguvu zao. (Sura ya 26, 10-11)



Msamaha na kuomba msamaha vinakomboa na kuifanya nafsi iwe yenye nuru.

Mtu aliye na uwezo wa kusamehe kila mara anapokosewa hailemei nafsi yake na hivyo anaumuondolea mwili wake mzigo wa uovu wote ule. (...)

Amri ya hukumu inasema hivi: Utahukumiwa kwa mjibu wa uzito na kipimo unachokitumia kwa wengine. Hayo yana maana kwamba ni kiwango cha uovu wa hisia, mawazo, maneno na matendo yako ndicho hakimu wako bali si Mungu. (Sura ya 57, 13-20)

«Samehe, nawe utasamehewa. » Ukiomba msamaha kwa jirani yako naye akikusamehe, Baba yako wa Mbinguni pia amekusamehe. (...) Ikiwa umeomba msamaha kwa jirani yako lakini bado hajawa tayari kukusamehe, neema ya Mungu itaongezeka ndani mwako, itakuzunguka na kukubeba, bila ya Mungu kukuondolea ouvu ambao bado haujarekebishwa. (Sura ya 26, 7-9)



Maandishi hayaleti uzima,
Ukweli unamweka mtu huru

Uaminifu kwa maneno matupu hudhihirisha kukosa imani kwa Mungu. Mtu asiyetekeleza Amri za Mungu hung'ang'ania maandishi. Ni kuamini maandishi huko ndiko kumesababishia ulimwengu machafuko. Hayo yametokea nyakati zote na kila mahali, na ni mamoja leo pia. (Sura ya 43, 10-16)

Yule anayelitimiza Neno la Mungu, amepewa pia wajibu wa kulitangaza ulimwenguni na kulifundisha. Lakini, wale wasiolitekeleza kimatendo wakae kimya. Maana anayelitangaza Neno la Mungu pasipo kulitekeleza huitwisha mzigo nafsi yake. Anatenda dhambi dhidi ya Neno Takatifu, dhidi ya Mungu. Maneno ya mtu ambaye anayeridhika kuhubiri na kufundisha Neno la Mungu bila kulitimiza, hayagusi moyo wa jirani yake. (Sura ya 76, 10-19)

Muda wote ambapo mtu hajatekeleza bado vipengele vyote vya ukweli wa milele ambavyo amefunuliwa, anavizingatia na kuvibaini kwa mjibu wa akili. Ni mara tu atakapotenda

hatua kwa hatua mambo aliyoyatambua ndipo atakapopata ujuzi wa ukweli mkuu sana. (Sura. 90, 6-11)

Kuomba kwa hali nzuri

Unapoomba, ingia katika chumba chenye ukimya na ingia ndani mwako, kwa kuwa Roho wa Baba ambaye wewe ni hekalu lake, anakaa ndani mwako. (…)

Ikiwa sala zako hazitiririki toka moyoni mwako bila ubinafsi, pahali pa kuomba, ni vema kutambua kwanza fikra na tamaa zako za kiutu ili uzinitolee hatua kwa hatua. Kwa hiyo, upendo usio na ubinafsi ulio ndani mwako utakua na utafikia kuomba kupitia moyo wako. (Sura. 26, 3-4)



Njia ya kiroho iongozayo kwenye moyo wa Mungu

Nilipochukua mwili katika Yesu wa Nazareti, nilitangaza Injili ya upendo inayoweka mtu huru, na ninaitangaza tena kama Kristo, kupitia wale wanaotimiza mapenzi ya Mungu. Kila mmoja anaweza kunipata katika njia ielekeayo kwenye uzima wa Kiroho ambayo nilionyesha na ninayoonyesha walio Wangu. (Sura. 13, 1-2)

Jueni kwamba katika Sheria ya milele hamna shuruti. Mungu, Wamilele, aliwatolea wanae wote uamzi huru. Yule anayechukua uamzi huru wa kufuata Kristo anapokea nguvu ya kutekeleza sifa za ukristo halisi: usawa, uhuru, umoja, undugu na haki. Sharti yote hutokana na kanuni ya kupanda na kuvuna, inayoitwa pia «Kanuni ya anguko». Ni vema mwanadamu achague njia yake ya kiroho kwa hiari yake mwenyewe. Mimi, Kristo, ninampendekezea kila mmoja njia iongozayo kwenye moyo wa Mungu, ila simlazimishi mtu awayeyote kuifuata. (…)

Madhehebu tofauti inayojidai ya Ukristo inalazimisha waumini wao kubatizwa kwa maji.

Kupitia tendo hilo, watoto wadogo ambao bado hawajakuza kiwango cha uamzi huru na hawawezi hivyo kuamua wenyewe, wanalazimishwa kuwa wanamemba wa Kanisa. (Sura. 25, 8)

Mafundisho ya Yesu mlimani, ikitekelezwa, ni njia ya kiroho iongozayo kwenye moyo wa Mungu. Jambo ambalo mtu hafanyi bila ubinafsi, analitenda tu kwa manufaa yake yeye mwenyewe. Kuto kulenga faida, ndio upendo wa Mungu. Ubinafsi ni upendo wa kibinadamu. Yule anayemtendea wema mwenziwe tu kusudi huyo anamshukuru na kumsifu kwa matendo yake mema, hatendi hivyo kwa ajili ya jirani yake, bali ni kwa ajili yake yeye mwenyewe. Shukrani na sifa ndiyo malipo yake. Hivyo tayari, amekwisha pokea malipo yake na hatapokea ingine toka Mungu. Ni kutenda bila kutegemea faida ndiko tu kunalipwa na Mungu. Hatua za kwanza kuelekea upendo bila ubinafsi ni kuchunguza fikra. Badili fikra za ubinafsi, fikra hasi, zenye giza,

za jeuri na fikra chanya, za usaidizi, za furaha na fikra safi na hata pia na fikra zenye mwelekeo kwenye mambo mema ndani ya kila mtu na ndani ya yanayokujia. (Sura. 26, 1-2)

Utajiri wa ndani na utajiri wa nje

Anayejishughulisha tu na raha yake mwenyewe, anayejenga «kiota chake», hashakii kwamba ndege wa mawindo tayari anakimbilia kukiharibu na kuchukua mali yake anayoiita miliki «yake».

Lakini, yule anayetafuta kwanza Ufalme wa Mungu hukuza maadili ya ndani, anakusanya hazina za kiroho. (…) Mtu ambaye ni tajiri wa kiroho hataishi katika mahitaji ya kimwili. Ila, yule ambaye ni tajiri wa kimwili na ambaye anakusanya utajiri huu, siku moja atakuwa na uhitaji. (Sura ya 26, 12-14)

Kila mwanadamu ni mwana wa Mungu na hatakiwi kuishi duniani kama ombaomba. Wala si vema kwa mtu yeyote kuishi katika anasa kubwa na utajiri na kuwaacha wengine wafanye kazi ili kukidhi raha yake yeye

mwenyewe tu. Hakika, kila mtu lazima atimize amri «Omba na ufanye kazi». Kila kazi inastahili mshahara wake. Anayefanya kazi kwa uaminifu pia ni mwadilifu kwa jirani yake. (Sura ya 47, 10-17)

«Omba na ufanye kazi»

Tambua kwamba kulingana na Amri za Wamilele, wote wanaotekeleza amri «Omba na ufanye kazi» bila ubinafsi wana haki sawa, kwa sababu Mungu humpa kila mtu kile anachohitaji na vya ziada tena. Lakini, amri hiyo itakapoendelea kutoheshimiwa na wote, kutakuwako duniani wale wanaoitwa matajiri. Kazi yao ni kugawa mali walizokusanya na kuishi kama wale ambao bila ubinafsi wanatimiza amri «Omba na ufanye kazi.» Ikiwa, kwa njia hiyo, hawafikirii tena manufaa yao wenyewe bali manufaa ya wote, utajiri wa kiroho utajidhihirisha pia kwa nje. Kisha hakuna mtu atakayeteseka na njaa au uhitaji. (Sura ya 25, 5)

Sheria ya dunia
na haki ya kimungu

Eleweni kwamba, Mungu si sheria, bali ni haki. Mwanadamu ameweka kanuni za kidunia zinazomaanisha sheria kwake. Maadamu mtu hajui Sheria ya Uzima, haki, mara nyingi anaamini kwamba anatenda kwa njia ya haki. Walakini yeye hunaswa kila mara katika kanuni ya kupanda na kuvuna kwa sababu sheria ya dunia hailingani na haki kila wakati. Haki ya wanadamu siyo haki ya Mungu. (Sura ya 57, 13-20)

Wanaume na wanawake wote ni sawa

Tambueni kwamba, Uzima humo katika kila nguvu, katika nguvu inayotoa na pia katika nguvu inayopokea. Ndio maana wake wanapaswa kuheshimiwa sawa sawa na wanaume. (...) Anayemchukua mwanamke kama mtu duni na kumthamini mwanamume kuliko yeye, anatenda kinyume na Sheria ya Uzima, kinyume na kanuni ya Baba-Mama

ambayo ni Sheria ya ulimwenguni kote. (Sura ya 64, 1-3)

Tendo la Kristo la ukombozi kutoka kwa Mungu

Mimi ndiye Mwana wa kwanza aliyezingatiwa na Baba, mzaliwa wa kwanza, ntawala pamoja na Baba wa Mbinguni, aliye pote katika nguvu nne za uumbaji, nguvu nne za msingi za Mungu: Mpango, mapenzi, hekima na unyofu. (...) Hivyo, Mimi ni Mungu katika Roho wa uumbaji wa Baba. (...) Mungu ndiye nguvu kuu, iliyo pote, iliyoumba kila kitu na inayoendelea kuuumba daima, ni nguvu iliyo milele na milele.

Nilichukua sehemu kubwa ya urithi Wangu wa kiroho ili kuipandikiza katika nafsi kupitia cheche Kutoka kwa nguvu hiyo iliyo pote, kutoka kwa uwezo wa msingi unaotiririka milele, ambao ni Roho. (...)

Baba wa Milele, ambaye Mimi ni Mwanaye, alinipa Mimi nguvu ya kufanya mapenzi yake, katika Sheria ya Milele: kuhifadhi uadilifu wa

kila kiumbe. Kupitia tendo la ukombozi, kila nafsi iliyolemewa sana ilipokea cheche ya ukombozi. Kwa hivyo, nafsi iliungwa mkono, ikalindwa na haiwezekani kuyeyuka katika Roho aliye pote, mkondo wa Mungu, haiwezi tena kutiririka humo kama nguvu za kitu kioevu. Kupitia ukombozi, nafsi itakuwa tena kiumbe safi cha kiroho na itabaki na hali yake ya kiroho kama mtoto wa Mungu. (...)

Kwa hiyo Baba amenipa Mimi wajibu wa kutenda kama Mkombozi wa roho zote na watu wote wenye kulemewa na mizigo na kuwaongoza kwenye moyo wake, wao ambao ni watoto wake. Hiyo ndiyo sababu Mimi nipo Mkombozi wa kila nafsi, hadi muda ambapo itakapofaulu kutambuka ngazi nne za utakaso. (Sura ya 20, 5)



Mwisho wa vikundi asilia miaka 2000 iliyopita

Baada ya kupaa Kwangu Mbinguni, kazi za ukuhani zilianzishwa pole pole. Wafanya huduma huo walitumia zaidi uwezo uliotolewa na kazi hiyo kiasi kwamba watu wengi waliojiunga na mitume na wanafunzi, na ambao hatua kwa hatua waliunda mashirika, walihitaji kuongozwa. Baadhi ya wanafunzi (...) hatua kwa hatua walianzisha mambo ya kipagani katika mashirika changa ya Kikristo.

Hivyo ndivyo hatua kwa hatua ule unaojidai Ukristo unaotegemea ibada na sherehe ya nje na uongozi wenye ngazi za madaraka ya wenye uwezo uliendelea, yaani uongozi wa wenye vyeo vikuu na waheshimiwa. Sijawahi kuanzisha ukristo huo kama Yesu wa Nazareti au kama Kristo wa Mungu.

Tambua kwamba mkuu kati ya walio Wangu ni yule aliyekuza «jiwe la kifalsafa» ambalo ni dhamiri safi ya ndani ya nafsi. Yeye ni mhudumu asiye na ubinafsi kwa manufaa ya wote. (...) Sikuwapa madaraka wainjilisti, wala mashemasi, wala makuhani. Nilitaka na

ninataka tu kundi moja ambalo Mimi, Kristo, ndiye Mchungaji wake. (...) Sikuanzisha ukuhani pia, lakini tu kikundi cha watumishi wasio na ubinafsi katika huduma kwa wote. (Sura ya 96, 6-7)

Unyanganyi wa madaraka ya jina la Yesu Kristo

Waakilishi wengi wa mamlaka ya kikanisa na wale wa ulimwengu huu hufanya siasa na kutumia sifa ya «Kikristo» kwa malengo isiyohusiana na ukristo. Wanatumia Jina langu kwa kutukuza lao. Wanafundisha watu injili ya upendo lakini ni wachache sana baina yao wanaoiishi. Wanatangaza sheria nyingi ambazo ni kinyume cha Sheria ya kimungu na hivyo kukanyaga kilicho kitakatifu zaidi, Sheria ya upendo na Uzima. Wanaruhusu wanyama wauawe. Wanakula nyama nyingi na kunywa vinywaji vikali. Wengi wao wana sehemu fulani ya uwajibikaji katika uharibifu, unyonyaji wa dunia na kujazwa sumu kwake. Na wengi wanaojiita wakristo wanachukua silaha kwa ajili ya vita. (...)

Hata leo, viongozi wa kikanisa huketi kwenye nafasi za heshima katika karamu makanisani kwao, na kuvikwa vyeo vya heshima na waamini wao. Hata leo, wanamheshimu mtu kwa cheo cha «Baba Mtakatifu», ingawaje nilipofanyika mwili katika Yesu wa Nazareti nilifundisha kwamba kuna Baba Mtakatifu mmoja tu. (Sura ya 60, 1-18)

Mchungaji Mwema huenda kutafuta kila kondoo Wake

Mchungaji mwema anawajua kondoo wake wote. (...) Kama Yesu wa Nazareti, Nilitoa maisha yangu ya duniani kwa ajili ya watu wote. Kama Kristo wa Mungu, Nilitoa urithi wangu mtakatifu kwa roho zote na watu wote ili kuwaunga mkono na kuwaongoza hadi kwenye nyumba ya Baba.

Kama cheche ya ukombozi, miale ya nuru kutoka kwa urithi wangu wa kiroho, sasa inaangazia roho zote na watu wote, wote watapata njia ya kurudi kwa Baba wa milele. (...)

Mimi, Kristo wa Mungu, namtafuta kila kondoo aliyepotea, kwa maana kila kondoo ni sehemu yangu. Hakuna mtu au nafsi iliyopotea milele. (Sura ya 55, 1-16)

Kristo hayuko tena duniani ndani ya Yesu; Kristo, ee mwanadamu, yu ndani mwako! Na popote ulipo, popote uendapo, Mimi ni nguvu ya ukombozi ndani mwako ambayo inaweza pia kuponya mwili wako ikiwa ni nzuri kwa roho yako. Ewe mwanadamu, huna haja ya kunitafuta, unanipata ndani mwako! Hakuna haja ya kwenda hapa au pale, niko ndani mwako! Popote ulipo, Mimi nipo pia. (...)

Na ikiwa hutaacha nafasi kwa shaka katika imani yako kwangu, chote kilicho kizuri kwako kitatokea, kizuri kwa wokovu wa nafsi yako. Leo kama jana, kanuni hii ina umuhimu: Imani yako imekusaidia. Na ukiacha kutenda dhambi kwa kujitahidi kuheshimu amri za Uzima, maombi yako tayari yamejibiwa nafsini mwako. Na wokovu utatiririka nafsini na mwilini mwako, ikiwa utatumikia maendeleo ya nafsi yako. (Sura ya 22, 1-5)





Yesu wa Nazareti alikuwa nani?

Utoto na ujana wake

Kitabuni humu mumekusanywa vifungu tofauti vya ufunuo wa Kristo, ambamo mwenyewe anaeleza hadithi ya maisha yake duniani katika Yesu wa Nazareti, kwa upekee ujana na utoto wake.

S170SW • ISBN 978-3-96446-226-8 • Kurasa 46



Jifunze kuomba

Katika sala ya kweli, unapata maarifa ya Mungu

Sala halisi humfanya mtu awe mwenye raha

Ila, sala halisi huhitaji mafunzo, kwa kuwa sala halisi, tunayoifanya ndani mwetu wenyewe, ni mazungumzo na Mungu.

S174SW • ISBN 978-3-96446-225-1 • Kurasa 54



Amri Kumi za Mungu
zilizotolewa kupitia Musa

Ni mashauri ya uzima yenye thamani kubwa inayomwezesha mtu kupata Amani ya roho, uhuru na kumsaidia kumkaribia hauta kwa hatua Mungu, Roho huru aliye ndani mwetu na ndani ya viumbe vyote.

S338SW • ISBN 978-3-96446-227-5 • Kurasa 46



Roho huru – Mungu ndani mwetu

Kitabu hiki kinamwelekeza msomaji kwenye njia ya uhuru na kinamuwezesha kujitenga na imani potovu, mila ngumu na taasisi zinazotushikilia. Njia hiyo ni njia iongozayo kwa Mungu, kwa Mungu ndani mwetu.

S179SW • ISBN 978-3-96446-247-3 • Kurasa 76

Vijitabu vitolewavyo bila malipo

- Kumpata Mungu! Wapi? Na Vipi?
- Usikate tamaa! Stahimili!
- Mungu ndani mwetu
- Mafundisho ya Yesu Mlimani
- Mnaishi milele. Hakuna mauti
- Uwezekano wa kuzaliwa upya katika mwili wa mwanadamu ni neema ya Uzima





Amri Kumi za MUNGU & Mafundisho ya Yesu wa Nazareti Mlimani

Gundueni Amri Kumi za Mungu zilizofafanuliwa katika usemi wa siku hizi na pia maelezo kuhusu Mafundisho ya Yesu Mlimani iliyofunuliwa na Kristo mwenyewe kupitia Gabriele, nabii na mjumbe wa Ufalme wa milele. Ni maadili ya ulimwenguni pote isiyotegemea dini na inayomlenga kila mmoja aidhuru utamaduni wake. Jaribu mwenyewe, ikiwa inawezekana, kubadili maisha yako.

S182TBSW • ISBN 978-3-96446-289-3 • Kurasa 228

Vitabu hivi vinapatikana pia katika lugha ya kiingereza, kifaransa na nyingine nyingi pia

Infos at WhatsApp/Viber in English: +49 151 1883 8742
Infos par WhatsApp en français: +49 159 08 45 45 05
www.gabriele-publishing.com

Hili ni Neno Langu
A na Ω

«Hili ni Neno Langu – A na Ω» ni kitabu kinachoeleza mawazo na kazi ya Yesu wa Nazareti ambaye tunamgundua kama nabii mashuhuri sana kuliko manabii wote wa Mungu na isitoshe, aliyekuwa Mwalimu mkuu.

Katika mabadiliko hii ya enzi, ni Kristo mwenyewe ndiye alifunua kupitia unabii wa Gabriele, nabii-mwalimu, ukweli wote kuhusu mafundisho na maisha yake duniani katika Yesu wa Nazareti. Anaeleza tena kwamba hajawahi kuunda dini wala kuwakabidhi makasisi madaraka.

Gabriele Publishing
The Word

Max-Braun-Straße 2 • 97828 Marktheidenfed • Germany

www.gabriele-publishing.com